



## ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21- 31 JANUARI, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 FEBRUARI, 2023.**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21- 31 JANUARI, 2023.**

Katika dekad hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) haikua na mabadiliko wakati ile iliyopo Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo. Hali iliendelea kuusukuma ukanda wa mvua juu kidogo kuelekea maeneo ya kusini na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua juu kidogo ya wastani hali iliyosababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa katika maeneo hayo. Katika tabaka la chini upepo uliendelea kuvuma kutokea Magharibi hususani katika nusu ya kwanza ya dekad, hali inayoendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Kongo kuelekea magharibi mwa nchi yetu. Hali hii ilikuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi, maeneo ya kati mwa nchi, ukanda wa pwani, ukanda wa kusini, na ukanda wa Ziwa Victoria. Pia kuimarika kwa wimbi anga katika bahari ya Hindi (*MJO*), katika nusu ya kwanza ya dekad kulichangia katika upatikaniaji wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21- 31 JANUARI, 2023.**

Kwa ujumla, katika nusu ya kwanza ya dekad hii maeneo mengi ya nchini yalipata mvua zilizoambatana na ngurumo za radi kufuatia uwepo wa migandamizo midogo ya hewa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hata hivyo, maeneo mengine yalipata mvua nyepesi katika dekad hii.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2023.**

### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2023.**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo wakati ile iliyopo Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo. Hali ambayo inatarajiwa kuusukuma ukanda mvua juu kidogo kuelekea Kaskazini kwa baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Mashariki mwa bahari ya Hindi wakati kusini Magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa wastani hadi chini ya wastani. Katika tabaka la chini upepo unatarajiwa kuendelea kuvuma kutokea Magharibi hususani katika nusu ya kwanza ya dekadi, hali inayotarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi yetu. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa pwani, kusini, kati na ukanda wa Ziwa Victoria hasusan katika nusu ya kwanza ya dekadi.

### **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE (01 - 10 FEBRUARI, 2023).**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):**

Vipindi vya mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi

vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar**

**es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo katika maeneo machache vinatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi vya mvua na ngurumo

za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vichache vya mvua na ngurumo za radi

katika maeneo machache vinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):**

Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika

maeneo machache vinatarajiwa.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya mvua

na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa

Imetolewa na;

## **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**